

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA**



**Simu ya Maandishi: DISCO MPWAPWA.**  
**Simu ya Mdomo: 026- 2320122/2320152/2320795.**  
**Fax Na. 255 - 026 - 2320122/2320152.**

S. L. P.12  
**MPWAPWA.**

13/05/2017.

**TANGAZO LA ZABUNI.**

**ZABUNI NA. LGA/023/2017/2018/G/W/NC/01.**

Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa imetenga fedha kutoka kwenye bajeti yake kwa ajili ya Manunuzi mbalimbali ya **Kazi, Vifaa na Huduma** kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa anakaribisha maombi kutoka **Makampuni, Vikundi na Wananchi** wenye sifa na uwezo wa kutekeleza zabuni mbalimbali kama ifuatavyo;-

**NB:** Tathmini (Evaluation) kwa waombaji zabuni namba **01 - 05** utakuwa wa awali (Pre - qualification).

<b>A: Ugavi wa vifaa mbalimbali:</b>		
01	Ugavi wa gesi (LPG Gas) katika vituo vya Afya na Zahanati.	LGA/023/2017 - 2018/G/01
02	Ugavi wa zana na pembejeo za kilimo.	LGA/023/2017 - 2018/G/02
<b>B: Utoaji wa huduma na kazi mbalimbali:</b>		
03	Kazi ndogondogo za ujenzi wa barabara na madaraja.	LGA/023/2017 - 2018/W/01
04	Kazi ndogondogo za ujenzi wa miundombinu ya maji, matanki ya maji, nyumba za pampu, ugavi wa pampu, mabomba na viungio.	LGA/023/2017 - 2018/W/02
05	Kazi ndogondogo za ujenzi wa majengo na majosho.	LGA/023/2017 - 2018/W/03
06	Pango kwenye vibanda vya biashara vya halmashauri ndani ya soko kuu Mpwapwa.	LGA/023/2017 - 2018/NC/01

07	Pango kwenye nyumba za biashara za Halmashauri zilizoko stendi ya zamani.	LGA/023/2017 - 2018/NC/02
08	Pango kwenye jengo la MPWADECO.	LGA/023/2017 - 2018/NC/03
09	Pango kwenye bucha za halmashauri eneo la soko kuu Mpwapwa mjini.	LGA/023/2017 - 2018/NC/04
10	Pango kwenye nyumba ya biashara eneo la forest - Mpwapwa mjini.	LGA/023/2017 - 2018/NC/05
11	Pango kwenye jengo la mgahawa wa halmashauri.	LGA/023/2017 - 2018/NC/06
12	Pango kwenye vibanda vya biashara vya halmashauri vinavyozunguka eneo la kituo kikuu cha mabasi - Mpwapwa mjini.	LGA/023/2017 - 2018/NC/07
13	Pango kwenye vibanda vya biashara vya halmashauri eneo la Mti mkubwa 'A' - Mpwapwa mjini.	LGA/023/2017 - 2018/NC/08

### Masharti ya Mwombaji:

1. Kila mwombaji atalazimika kulipia **Tshs. 50,000/=** kwa kila zabuni itakayo ombwa. Na malipo hayo yatafanywa kupitia akaunti namba **50410000579** (MDC Own Source Rev. A/C) baada ya kupatiwa ankara ya malipo toka ofisi ya Mweka hazina.
2. Halmashauri ya wilaya haitalazimika kukubali zabuni ya chini kabisa au ya juu.
3. Mwombaji awe na leseni hai ya biashara ya aina ya zabuni anayoomba, pia atatakiwa kuambatanisha vitu muhimu kama ilivyoainishwa kwenye kitabu cha zabuni.
4. Ada ya maombi haitarejeshwa na stakabadhi ya ada ya maombi iambatanishwe kwenye kitabu cha maombi ya zabuni husika.
5. Kwa waombaji wa zabuni za upangaji kwenye vibanda vya biashara na nyumba za biashara za halmashauri waonyeshe ni kiasi gani watailipa Halmashauri kwa mwezi.
6. Kwa zabuni za ugavi wa bidhaa mbalimbali, mwombaji atoe orodha ya bidhaa muhimu na bei kwa kipimo cha 'unit' moja kulingana na zabuni husika.
7. Kwa waombaji wa zabuni za mchujo wa awali wa ukandarasi waambatanishe cheti cha usajili wa kampuni kutoka bodi ya wakandarasi, leseni, TIN No, orodha ya kazi ambazo Mkandarasi alishawahi kufanya, orodha ya zana za kazi, nakala ya taarifa ya fedha (Bank statement/Audited financial statement) na maelekezo mengine kama yalivyoainishwa kwenye kitabu cha zabuni husika.

8. Mwombaji atatakiwa kutaja Wakurugenzi/Mkurugenzi wa kampuni, mahali ofisi ilipo na aambatanishe 'company profile'.
9. Vigezo vya tathmini ya zabuni ni kama ilivyoainishwa kwenye tangazo hili na kwa mujibu wa kitabu cha zabuni husika.
10. Mwombaji atoe tamko la kutojihusisha na vitendo vya rushwa.
11. Maombi yawekwe kwenye bahasha iliyofungwa kwa lakiri (seal) na juu ya bahasha iandikwe kwa herufi kubwa aina ya zabuni anayoomba na itumwe kwa anuani ifuatayo;-

**KATIBU, BODI YA ZABUNI,  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
S.L.P 12,  
MPWAPWA.**

12. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **2/6/2017** saa **4.00** asubuhi na zabuni zitafunguliwa siku hiyo hiyo saa 4.00 asubuhi kwenye ukumbi wa halmashauri ya wilaya ya Mpwapwa. Waombaji au wawakilishi wa waombaji wanakaribishwa kuhudhuria kwenye ufunguzi.

Mohamed A. Maje  
**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
MPWAPWA.**